



USHAURI WA SERA

Shughuli za Nje 2024 - 2

Sera: Kufunga Maombi Yaliyotelekezwa katika Usimamizi wa BRC

Tarehe ya Kuanza: Februari 1, 2024

Kiungo cha Sera: <https://www.mass.gov/doc/eec-closing-abandoned-requests-in-brc-manager-policy-documentswahili/download>

MUHTASARI

Ili kuhakikisha kuwa orodha ya maombi yanayosubiri ya Ukaguzi wa Rekodi ya Historia (BRC) ni ya sasa na inajumuisha waombaji tu ambao wamechukuliwa alama za vidole, EEC itafunga maombi ya BRC katika mfumo wa Usimamizi wa BRC siku 120 baada ya kuwasilishwa ikiwa mwombaji atakuwa hajatoa alama za vidole kufikia wakati huo.

Sera hii itaathiri maombi ya BRC kwa waombaji wote waliopo, ikijumuisha wale waliopo katika hali yenye masharti au ya kusasishwa. Waombaji walio katika hali yenye masharti au ya kusasishwa ambao BRC yao imefungwa kwa mujibu wa sera hii lazima waondolewe kwenye mpango ndani ya siku 14.

MATUMIZI

Sera hii inatumika kwa mipango yote yenye leseni na/au iliyofadhiliwa.

SASISHO MUHIMU

- EEC itafunga maombi ya BRC yaliyotelekezwa katika mfumo wa Usimamizi wa BRC baada ya siku 120 ikiwa haijatiwa alama za vidole.
- Mwombaji yeyote ambaye ana ombi la BRC katika mfumo wa Usimamizi wa BRC ambalo ni la siku 120 au zaidi, ana hadi Januari 31, 2024 ili achukuliwe alama za vidole kabla ya sera hii kuanza kutumika tarehe 1 Februari 2024.
- Sera hii inatumika kwa waombaji ambao wako katika hali ya kusubiri, yenye masharti au ya kusasishwa. Mwombaji yeyote ambaye kwa sasa anafanya kazi katika mpango wenye leseni au unaofadhiliwa na BRC katika hali yenye masharti au ya kusasishwa, ambao BRC yake imefungwa kutokana na sera hii, lazima aondolewe kwenye mpango ndani ya siku 14.
- Waombaji ambao BRC yao imefungwa kwa sababu ya sera hii lazima wawasilishe upya maombi mapya ikiwa wangependa kutuma ombi tena na hawawezi kufanya kazi au kushirikiana na mpango wowote hadi watolewe uamuzi wa ufaafu.

RASILIMALI

[Tafadhali angalia mwongozo wa nyenzo za EEC kuhusu sera hiji](#). Iwapo wewe au wafanyakazi wako mna maswali kuhusu sera hii au mnahitaji usaidizi wa ziada, tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha EEC katika 617-988-7841.

ISİYOTUMIKA

Hii ni sera mpya na haichukui nafasi ya sera zozote za sasa za EEC BRC.